

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



Dodoma
06 Mei, 2026

Barua pepe: press@ikulu.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

RAIS SAMIA AWAAPISHA VIONGOZI WATEULE, IKULU CHAMWINO

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo amemuapisha Mhe. Dkt. Evaline Wilbard Munisi (Mb.) kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma.

Rais Dkt. Samia amesema uteuzi wa Dkt. Munisi, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa NCCR-Mageuzi, umetokana na sifa, uwezo na uzoefu wake katika masuala ya umma na mahusiano, akisema Watanzania wote wana wajibu wa kuunganisha nguvu katika kulitumikia Taifa bila kujali tofauti za itikadi za vyama.

“Evaline ni Katibu Mkuu wa chama cha upinzani cha NCCR-Mageuzi; lakini nimeangalia wasifu wake, nikaona ana sifa za kuingia ndani ya Serikali na kutusaidia,” amesema Rais Dkt. Samia.

Halikadhalika, amemtaka Dkt. Munisi kushirikiana na viongozi na watendaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano kusimamia kazi zenye staha, haki na stahiki za wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi, pamoja na juhudi za kutafuta na kulinda fursa za ajira kwa vijana wa Tanzania nje ya nchi.

Amesema Ofisi hiyo pia ina jukumu la kuimarisha mahusiano kati ya Serikali, waajiri na waajiriwa, pamoja na mahusiano ya kuheshimiana baina ya Serikali na mihimili mbalimbali ya dola.

Kwa upande wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), Rais Dkt. Samia amemtaka Mtendaji Mkuu Dkt. Kheri Mahimbali kusimamia vyema taasisi hiyo ili kurejesha ufanisi na imani yake kwa umma, hususan baada ya hoja na changamoto zilizoibuliwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).



Rais Dkt. Samia amewataka viongozi hao kutekeleza majukumu yao kwa nidhamu, unyenyekevu na matokeo, akisisitiza kuwa dhamana ya uongozi inapaswa kuelekezwa katika kutatua changamoto za wananchi.

“Vyeo ni dhamana. Mungu amekuweka hapo ili utumikie watu,” amesema Rais Dkt. Samia.

Viongozi wengine walioapa kiapo cha uadilifu kwa watumishi wa umma ni: Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Ndugu Kheri Abdul Mahimbali; Katibu wa Rais, Balozi Ali Jabir Mwadini; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi Peter Philip Mwasalyanda; Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Dkt. Jabir Kuwe Bakari; na Mshauri wa Rais, Masuala ya Jamii, Mhe. Angela Charles Kizigha (Mb.).



Bakari S. Machumu

Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu